

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Eliurd Mwaiteleke amewataka Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Misungwi hususan Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji pamoja na Idara ya Mifugo na Uvuvi kutumia vyema fursa za Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Mifugo zinazotolewa na Taasisi za Umma zilizopo Wilayani Misungwi.

Akizungumza na Wakuu wa Taasisi za Utafiti wa Kilimo na Mifugo Wilayani hapa mapema hii leo wakati wa ziara yake alipozitembelea taasisi hizo kwa lengo la kujitambulisha na kupanga Mikakati mbalimbali ya maendeleo kwa kushirikiana na taasisi husika pamoja na mambo mengine hakufurahishwa na suala la kutozitumia kikamilifu fursa za kuwepo Taasisi muhimu za Kituo cha Utafiti wa Kilimo Ukiriguru, Chuo cha Mafunzo ya Kilimo Ukiriguru, Shamba la Uzalishaji wa Mifugo la Mabuki, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mabuki pamoja na Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Mabuki, alisema kuwa katika taasisi hizo kuna fursa nyingi sana endapo zitatumwa vizuri na Watendaji wa Halmashauri katika kusukuma maendeleo kuititia Nyanja za Kilimo bora na Ufugaji wa kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji, Mwaiteleke ameweke bayana Vipaumbele vya Halmashauri katika juhudini za kukuza Uchumi wa wilaya ambavyo ni pamoja kufufua Kilimo cha Zao la Pamba na kuanzisha Kilimo cha Alizeti ikiwa ni zao la biashara pamoja na kusindika Mafuta yatokanayo na Alizeti na Menejimenti imejipanga kutoa mbegu za Alizeti kwa kuwakopesha Wakulima watakaolima ambapo tayari Maafisa Ugani na Watendaji wa Kata na Vijiji wanaendelea na Utoaji wa Elimu na kuhamasisha Wananchi na kuwaorodhesha ili kupata takwimu halisi ya mahitaji ya wanatarajia kulima Alizeti katika msimu huu.

Amewataka Wakuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo kuhakikisha wanatoa Ushirikiano wa kutosha kwa Wataalam na Watafiti wa Mazao mbalimbali walioipo kwenye taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ukiriguru na Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Mabuki ambazo ni chachu na nguzo imara katika utoaji wa Elimu na Mafunzo ya mbinu bora za Uzalishaji wa Mazao hususan zao la Pamba, Mpunga, Dengi, Mahindi sambamba na Alizeti kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija na faida kwa Wakulima Wilayani Misungwi.

Awali, wakitoa taarifa ya Mafanikio waliyoyapata kuititia utafiti wa kilimo wanaoufanya baadhi ya Watafiti akiwemo Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ukiriguru, Everine Lukonge alisema wameweza kubaini vipengele mbalimbali vya kuongeza thamani ya Mazao ikiwemo zao la Pamba, Mihogo, Ulezzi, Mtama, Mbazi, Dengi, Karanga na Alizeti ambayo yanafaa kwa asili ya udongo uliopo maeneo mengi ya Wilaya ya Misungwi.

Alitoa Mfano wa baadhi ya maeneo ya Vijiji viliviyofanyiwa utafiti na kufanikiwa kulima vizuri katka zao la Dengi ni Kijiji cha Iteja na Ilalambogo na upande wa utafiti wa Zao la Mtama na Uwele ambayo yalitekelezwa kama mradi wa Sukuma Vita kwa lengo la kurutubisha Udongo na kuondoa na kuondoa Kiduha kinachoshambulia Mazao mbalimbali, kuititia Mradi huu watafiti walitoa Ushauri wa kutumia mbegu za Mtama za WAHI na HAKIKA ambazo zilizalishwa na kulimwa katika Vijiji vya Ng'ombe na Mapilinga na mbegu hizo zilisambazwa katika Maeneo mengi hapa nchini.

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Misungwi, Eliurd Mwailteleke katika majumuisho ya ziara hiyo amewashukuru Wakuu wa Taasisi hizo na kuwaomba kuweka Mikakati ya pamoja ya kuboresha na kufufua Kilimo cha Mazao ya Pamba, Mtama na sambamba na kuimarisha Ufugaji Mifugo wa

kisasa wenyе kuleta tija na maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii ya Wasukuma kwa kujenga nyumba bora na hatimaye kuondokana na makazi duni .

Aidha, katika mipango ya Halmashauri amepanga kuandaa Mkutano hivi karibuni wa Wadau wote wa Sekta ya Kilimo na Mifugo katika Wilaya kwa lengo la kuweka Mikakati na Mipango madhubuti ya kuboresha Sekta ya Kilimo na Ufugaji kwa kuzitumia Taasisi zote za Umma na Mashirika binafsi yanojihusisha na Masuala ya Sekta hizo.

Imetolewa na:

Thomas Lutego

Kaimu Afisa Tehama na Uhusiano (W)

MISUNGWI

17 Oktoba, 2017